

Karatasi la maelezo 3: Kuhusu kupiga kura (uchaguzi wa Jimbo)

Katika Australia Magharibi, kuna nyumba mbili za Bunge.

Nyumba ya chini inaitwa Bunge la Kutunga Sheria. Inakuwa na wajumbe 59.

Kila mjumbe anachaguliwa kuwakilisha mojawapo ya wilaya 59 za uchaguzi.

Nyumba ya juu inaitwa Baraza la Kutunga Sheria.

Ina wajumbe 36, inavyokuwa wajumbe sita waliochaguliwa kwa kila mkoa wa mikoa sita ya uchaguzi.

Unapiga kura kwa wagombea ambao wanataka kuwakilisha wilaya au mkoa unapokaa. Washindaji wanakuwa wajumbe wako waliochaguliwa.

Wakati wa uchaguzi mkuu, unaombwa kupiga kura kwa mtu unayetaka akuwakilishe kwa:

- Wilaya yako ya Bunge la Kutunga Sheria
- Mkoa wako wa Baraza la Kutunga Sheria.

Utapewa makaratasi mawili ili upige kura.

Karatasi jeupe la kura inayokuwa ndogo zaidi ni kwa Bunge la Kutunga Sheria (wilaya yako).

Soma maelekezo kwa uangalifu.

Tumia nambari pekee.

Anza na nambari '1', ndipo weka nambari kwa boxi zote kwa mpango wa uchaguzi wako.

Karatasi la kura lenye rangi linalokuwa kubwa zaidi ni wa Baraza la Kutunga Sheria (mkoa wako).

Soma maelekezo kwa uangalifu.

Tumia nambari pekee.

Una uchaguzi mbili kwa kuweka alama kwenye karatasi lako la kura.

Unaweza kuandika nambari '1', ndani boxi karibu chama au kundi la uchaguzi wako juu ya mstari

au

Unaweza kuweka nambari kwa boxi zote chini ya mstari kwa mpango wa uchaguzi wako.



Unaweza kuomba afisa wa kura kukusaidia wakati wowote.

Kuwa mgombea

Ili kuwa mgombea, lazima uandikishwe kupiga kura.

Angalia ‘Kuhusu kuandikisha’ kwa maelezo zaidi jinsi ya kuandikisha.

Ili kujipendekeza utahitaji:

- Kujaza fomu ya mapendekezo
- kutolea habari zote zinazoombewa
- kulipa amana.

Kiasi cha amana ni tofauti na inategemea kama unapendekeza kwa uchaguzi wa serikali ya Jimbo, ya Shirikisho au ya mtaa.

Unaweza kujipendekeza wewe mwenyewe au kama mjumbe wa chama au kundi la siasa.

Kwa maelezo zaidi, enda kwa www.elections.wa.gov.au au pigia simu kwa 13 63 06 au (08) 9214 0400 kwa wapigiaji simu wa kuvuka majimbo.